



Badiliko Muhimu kwa Sera ya Kusimamisha Shule

Disemba 14, 2020

Salamu Wapendwa Familia za Lowell Public Schools,

Huku tukiwa na utabiri wa hali ya hewa ya kipupwe baadaye wiki hii, tungependa kuwasiliana na jamii yetu ya LPS na kugawa nanyi badiliko kwa Sera ya Kusimamisha Shule kwa mwaka wa shule huu.

Katika wakati uliyopita, iwapo kulikuwa na hewa yenye baridi kali, tulikuwa na chaguo za kuhairisha mwanzo wa siku ya shule, au kusimamisha shule na kuwa na “siku ya barafu”. Kamati ya Shule hivi karibuni ilikubali ongezeo la chaguo la tatu la kuwa na “Siku ya Mafunzo ya Mbali” kwa sera inayotumika sasa hadi Juni 30, 2021.

Chaguo hili mpya linatupatia unyambuliko wa ziada. Badala ya kuwa na siku ya barafu kaa zamani iwapo shule zetu zimefungwa kwa sababu ya hewa yenye barafu, tunaweza sasa kuwa na siku ya shule ya mafunzo ya mbali itakayohesabiwa kukamilisha idadi za siku za mafunzo zinazohitajika.

Uamuzi kuwa na Siku ya Mafunzo ya Mbali Kikamilifu itaathiri wanafunzi wote, bila kujali iwapo wao huhudhuria shule kibinafsi au husomea kwa mbali. Majengo ya shule yatakuwa yamefungwa katika Siku za Mafunzo ya Mbali Kikamilifu, na masomo yatatekelezwa nyumbani kwa wanafunzi wote. Wafanyikazi wa shule watawapatia wanafunzi taarifa zaidi kuhusu matarajio ya mafunzo katika Siku ya Mafunzo ya Mbali Kikamilifu kwa minajili ya hewa ya baridi kali.

Wakati mijengo ya shule imefungwa kwa sababu ya hewa yenye baridi kali, ikiwamo katika Siku ya Mafunzo ya Mbali Kikamilifu, sehemu za kuchukua chakula pia zitafungwa. Lakini, iwapo tutaweza kutabiri hewa kali, wanafunzi wataweza kupata vyakula vya ziada katika sehemu za kupokea chakula siku moja kabla yae. Tutawasiliana hili na familia kabla ya wakati huo.

Tutatangaza Siku ya Mafunzo ya Mbali Kikamilifu, kutokuwepo kwa shule, au kuhairisha kufungua kwa shule kupitia simu, barua pepe, tovuti la LPS na mtandao wa kijamii wa LPS. Tutagawa habari hii pia kupitia TV ya mtaa na vituo vya redio.

Asante kwa utegemezi wako na ushirikiano wako unaoendelea mwaka wa shule huu wote.